


ekari 14 kwa ajili ya ujenzi wa Kiwanda na kugharamia miundombinu ya barabara maji na umeme.

Faida zitakazopatikana kutokana na mradi huu ni pamoja na kupunguza taka katika masoko kwa tani 50 kila siku , uzalishaji wa tani 25 za mbolea kila siku, ongezeko la mapato ya Manispaa kutokana na mauzo ya mbolea, kupunguza matumizi ya mbolea zenye athari kwenye ardhi na afya ya binadamu na kuongezeka kwa fursa za ajira kwa Watanzania.

Aidha ushirikishaji wa Wadau ni moja ya hatua zilizozingatiwa katika uanzishwaji wa mradi huu kwa kutoa mawazo yao, kwa maendeleo endelevu ya mradi sambamba na kutoa fursa kwa wananchi kujua na ,kutambua kwa mapana athari za kimazingira na mabadiliko ya tabia nchi.

Mwisho Mstahiki Meya amewaeleza wadau wote na wakazi wa Kinondoni kwa ujumla kuwa Manispaa yake imeupokea mradi huu wa Kiwanda kwa mikono miwili na kwamba kwa namna ya pekee ametoa shukrani za dhati kwa Uongozi mzima, na wananchi wa Jiji la Hamburg na Serikali ya Ujerumani, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wizara ya Fedha na mipango, ofisi ya Rais TAMISEMI, kwa kufanikisha mchakato wa upatikanaji wa fedha za mradi huu. Pia aliwashukuru Wataalamu Dr. Florian Koelch mtaalamu mshauri, na mwakilishi wa Jiji la Hamburg Bw. Denis Machinik kwa kuratibu mkutano wa Wadau, kupitia kampuni ya Atmosfair na kwamba Manispaa ya Kinondoni itatekeleza mradi huu kwa nguvu zote ili malengo yaliyokusudiwa yaweze kufikiwa,



Sebastian M. Mhowera

**AFISA UHUSIANO WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI.**